

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA  
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

638


**VIELELEZO NA TEKNOLOJIA**

**Muda: Saa 3**

**Mwaka : 2021**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A na B zenye jumla ya maswali **kumi na sita (16)**.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A na maswali **manne (4)** kutoka sehemu B.
3. Sehemu A ina alama **arobaini (40)** na sehemu B ina alama **sitini (60)**.
4. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** ndani ya **chumba cha mtihani**.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha **kujibia**.



## SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. Kwa kutumia hoja nne, oneshwa ufanano kati ya vielelezo na teknolojia vya kukodi na vielelezo na teknolojia vya kuazima.
2. Bainisha hatua nne muhimu zinazopaswa kufuatwa na mwalimu wakati wa kufaragua zana kwa kutumia udongo wa mfinyanzi.
3. Eleza kwa kifupi manufaa manne ya kuwa na vielelezo na teknolojia imara katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.
4. Kwa kutumia zana nne, fafaua kwa kifupi dhana ya vielelezo na teknolojia mpitisho.
5. Kwa kutumia hoja nne, oneshwa sifa nne za vielelezo na teknolojia vya kisasa.
6. Fafaua kwa kifupi mambo muhimu manne ya kuzingatia wakati wa kufaragua na kutengeneza vielelezo na teknolojia vinavyokidhi umri na uelewa wa walengwa.
7. Eleza kwa kifupi dhana ya vielelezo na teknolojia mafunzo kwa kutumia zana nne.
8. Kwa kutumia mifano, fafaua tofauti mbili kati ya vielelezo na teknolojia tata na vielelezo na teknolojia rahisi.
9. Endapo umepewa jukumu la kununua ubao wa chaki kwa ajili ya kufundishia na kujifunzia, ni vigezo gani utatumia ili kupata ubao unaofaa. Eleza vigezo vinne.
10. "Nyimbo na sauti ni vielelezo na teknolojia masikizi ambayo husaidia kufikisha ujumbe kwa urahisi kwa wanafunzi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji." Thibitisha usemi huu kwa ufupi kwa kutoa hoja nne.

## SEHEMU B (Alama 60)

Jibu maswali manne (4) kutoka sehemu hii.

11. Maendeleo ya sayansi na teknolojia yameleta athari chanya na hasi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Kwa kutumia hoja tano, oneshwa athari hasi za matumizi mabaya ya mikanda ya video na CD.
12. Kabla ya kuanza kufaragua au kutengeneza zana za kufundishia na kujifunzia moja kati ya mambo ya msingi ni kufanya tathmini ya mada husika. Thibitisha kauli hii kwa kutoa hoja tano.

13. Ikiwa unafundisha katika shule ambayo walimu wengi hawazingatii utunzaji wa vielelezo na teknolojia, ni mambo gani utawaeleza walimu hao kuhusu umuhimu wa kutunza vielelezo na teknolojia? Eleza kwa kutoa hoja tano.
14. Kwa kutumia hoja tano, onesha namna mwalimu anavyoweza kuwasaidia watoto wenye uoni hafifu na wasioona kutumia vielelezo na teknolojia katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.
15. Eleza madhara matano yanayoweza kujitokeza endapo mwalimu atatumia zana pasipo kuzingatia msingi wa umri na uelewa wa wanafunzi.
16. "Matumizi ya vielelezo na teknolojia asilia humsaidia mwanafunzi kujifunza kwa kutumia milango mingi ya fahamu." Thibitisha kauli hii kwa kutoa hoja tano.